

Riwaya ya *Walenisi* na Uhalisi Wake katika Nchi Zinazoendelea

Gerephace Mwangosi

Ikisiri

Wanafasihi wanatumia mbinu za kisanii kuelezea masuala mbalimbali yanayosawiri hali halisi katika jamii zao. Miongoni mwa masuala yanayoelezwa ni athari za ukoloni mamboleo, ukosefu wa haki, uongozi mbovu pamoja na matabaka yaliyotamalaki katika jamii. Makala hii inajaribu kuelezea mchango wa dhamira za fasihii ya Kiswahili katika kujadili hali halisi ya maisha ya kila siku ya jamii hasa katika kipindi hiki cha sera za soko huria katika nchi zinazoendelea. Kwa kurejelea riwaya ya *Walenisi* ya Katama Mkangi (1995), makala inatalii hali halisi ya nchi zinazoendelea katika kipindi hiki ambapo hali ya uchumi, siasa na utamaduni, kwa kiasi kikubwa, inadhibitiwa na ubepari na mataifa yaliyoendelea. Aidha, makala inadokeza hali halisi, mwelekeo na matokeo ya sasa na yajayo katika nchi zinazoendelea. Data za makala hii zimepatikana kwa kusoma riwaya ya *Walenisi* na nyaraka nyinginez. Nadharia ya Uhalisia imetumika katika uchambuzi wa data. Makala inahitimisha kwamba kadiri mataifa ya kibepari yanavyotumia mbinu za hali ya juu kuhakikisha masilahi yao yanatimizwa, ndivyo uchumi katika nchi zinazoendelea, zikiwamo za Afrika Mashariki, unavyozidi kudhoofika na kuporomoka.

1.0 Utangulizi

Katama Mkangi alizaliwa mwaka 1944 huko Ribe katika mkoa wa Pwani nchini Kenya. Mkangi alikuwa mwanasosholojia aliyependa kuzungumzia masuala nyeti ya kijamii na kisiasa yaliyotawala wakati huo nchini Kenya. Mwaka 1986 aliwekwa kizuizini kwa tuhuma za kuhusika katika kikundi cha siri cha Wakenya waliotaka kuiangusha serikali. Hata hivyo, Wakenya wengi walielewa kuwa, sababu ya kuwekwa kizuizini ilitokana na msimamo na itikadi zake zilizoipinga serikali. Baada ya kuachiwa kutoka kizuizini, alinyimwa kazi katika vyuo vikuu vya serikali vya Kenya. Itakumbukwa kuwa katika uchaguzi mkuu wa mwaka 1997 aligombea kiti cha urais wa Jamhuri ya Kenya, lakini hakufaulu. Mkangi alifariki kwa ajali ya gari tarehe 7 Machi, 2004 akiwa mbunge huko nchini Kenya. Pamoja na *Walenisi*, riwaya zake nyingine ni *Ukiwa* (1975) na *Mafuta* (1984). Riwaya ya *Walenisi* inaanishi masuala kemkemu yanayoziathiri nchi zinazoendelea, ukiwamo ukandamizaji, matumizi mabaya ya sheria, kukosekana kwa haki na usawa, demokrasia na utawala mbaya.

Mkangi ametumia sanaa ya aina yake kuijenga riwaya yake ya *Walenisi*. Kupitia chombo kiitwacho sayari, anaonesha namna kinavyotumiwa na viongozi wadhalimu kama chombo cha kifo na maangamizi. Chombo kilichotumika kuondoa ujinga na umaskini, kikaanza kutumiwa na viongozi wa kiimla ili kuangamiza fikra chanya na mbadala zilizolenga kuchochea maendeleo ya umma. Chombo hiki kilitumika kuwakomesha wale wote waliopinga utawala wao. Dzombo anang'oa nanga katika sayari, chombo kilichotakiwa kumuua ghafla, hatimaye kilimpeleka katika ulimwengu mwingine. Ulimwengu huo mpya unakuwa ni funzo kwake. Chombo hiki cha kifo kilimwezesha kujitambua zaidi, kuielewa nchi yake na kuyaelewa mazingira yake kwa undani zaidi. Chombo hiki cha kifo kilimpa uhai wa aina fulani kwa sababu kiliamsa na kuupanua urazini wake. Nchi aliyopelekwa akiwa ndani ya chombo hicho ilikuwa nchi ya kufikirika iliyotazamwa kama kielelezo cha maendeleo katika nyanja za siasa, uchumi na maisha ya jamii kwa ujumla. Dzombo alihukumiwa kifo na mahakama ya nchi yake kwa madai kwamba amevunja sheria ya nchi. Kosa lilikuwa ni kudai haki yake na ya wafanyakazi wenzake. Matokeo yake alihukumiwa kifo kwa sayari, chombo cha kisayansi.

Katika safari yake sayarini, Dzombo alikabiliana na majabali mbalimbali. Majabali hayo ni taashira ya matatizo kemkemu yaliyotamalaki duniani. Baadhi ya matatizo hayo ni ujinga, magonjwa, udhalimu na kuimarika kwa kasumba ya tabia za kigeni. Dzombo alitua nchini *Walenisi* (Wale ni sisi na sisi ni wale), nchi inayooonesha muumano na ushirikiano wa binadamu. Akiwa *Walenisi*, Dzombo alijifunza utu, usawa kazini na uongozi bora unaofuata misingi ya demokrasia na katiba ya nchi. Mkangi anamtumia Dzombo kama mwanamapinduzi anayepinga dhuluma, unyonyaji na matabaka yaliyopo katika nchi zinazoendelea, kama Nyerere (1974) na Idrisa (2016) wanavyosisitiza kuwa, jamii haina budi kuishi kwa umoja na ushirikiano, usawa, uhuru na amani. Kwa upande mwingine, Mkangi anakosoa mfumo wa serikali na mbinu zake za uzalishaji mali ambazo hazina tija kwa ustawi wa uchumi wa jamii na taifa. Katika kuyabainisha yote haya, Mkangi anaonesha hali halisi ya matatizo yanayoathiri harakati za ujenzi wa jamii inayofuata misingi ya haki na usawa kwa manufaa ya umma. Kimsingi, makala hii imechunguza uhalisi wa dhamira za fasihi ya Kiswahili. Dhamira zilizochunguzwa katika makala hii ni ukoloni mamboleo, athari za matabaka na ukosefu wa haki katika nchi zinazoendelea, zikiwamo za Afrika Mashariki, pamoja na hitimisho.

2.0 Mbinu za Utafiti

Makala hii inajaribu kuelezea mchango wa dhamira za fasihi ya Kiswahili katika kujadili hali halisi ya maisha katika nchi zinazoendelea, zikiwamo za Afrika Mashariki na nyinginezo barani Afrika. Kwa kurejelea riwaya ya *Walenisi* ya

Mkangi (1995), makala inatalii hali halisi ya nchi zinazoendelea katika kipindi hiki ambapo hali ya uchumi, siasa na utamaduni, kwa kiasi kikubwa, inadhibitiwa na ubepari na mataifa yaliyoendelea. Riwaya hii ilichaguliwa kwa kuwa ina mawanda ya kutosha kuwakilisha data zinazohusiana na mada iliyoteuliwa na kuchunguzwa. Data za msingi zilipatikana kwa kusoma riwaya ya *Walenisi*. Aidha, data za upili zilipatikana kwa kusoma maandiko mbalimbali katika maktaba ya Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Ruaha iliyopo mkoani Iringa. Maktaba hii iliteuliwa kwa kuwa ina data za kutosha zilizohusiana na mada ya utafiti huu.

3.0 Uhalisi katika Fasihi ya Kiswahili

Uchambuzi wa data katika makala hii umeongozwa na Nadharia ya Uhalisia. Dhana ya uhalisi katika Nadharia ya Uhalisia hutumiwa kuelezea tapo la kifasihi ambalo huzitazama kazi za kifasihi kama zinaakisi sifa za kimsingi zinazohusishwa na uhalisi. Kwa kiasi kikubwa, kazi ambazo zinaangaliwa kama za kihalisa, zinatarajiwa kuwa kama akisiko la hali halisi ya maisha katika jamii inayohusika. Uhalisia husisitiza uwasilishaji wa maisha ya jamii kwa uaminifu na usahihi mkubwa (Wamitila, 2002). Nadharia ya Uhalisia inadhihirisha hali halisi iliyopo katika nchi mbalimbali. Kwa kufanya hivyo, msisitizo mkubwa uliwekwa kwenye ukweli uliopo katika nchi zinazoendelea zikiwamo za Afrika Mashariki hasa ukichunguza dhamira zilizobainishwa katika riwaya iliyochunguzwa.

3.1 Ukoloni Mamboleo

Katika kuenzi asili, hakuna ustaarabu wowote duniani ambao kufikia sasa umejengwa katika misingi ya kuiga ustaarabu wa watu wengine; na sisi tulioko barani Afrika hatuhitaji kuiga falsafa za wengine, tabia, mienendo na utamaduni wao ili tuwe wastaarabu (Mihanjo, 2010). Utamaduni ni mwenendo wa maisha ya jamii, mtazamo wa mambo na taratibu zao za kuendesha maisha zinazowatofautisha wao na jamii nyingine (Makoye, 1996 na Ipara, 2003). Utamaduni ndicho kitambulisho kikuu cha taifa lolote, na ni kielelezo cha utashi na uhai wa watu wake. Taifa bila utamaduni ni kama taifa bila fahamu na lisilo na mwelekeo wa maisha yake (Sengo, 1993). Kwa misingi hiyo, kila jamii ina wajibu wa kuulinda, kuuendeleza, kuuhifadhi na kuuensi utamaduni wake.

Kadiri muda unavyopita, ndivyo mifumo ya maisha katika nchi za Afrika Mashariki na kwingineko barani Afrika inavyozidi kubadilika huku baadhi ya mila na desturi zikionekana kupitwa na wakati (Mgogo, 2012). Hapana shaka kwamba, ukoloni mamboleo umeathiri kwa kiasi kikubwa misingi ya ukuaji na uendelevu wa utamaduni, siasa na uchumi katika jamii za Kiafrika. Hali hiyo inatokana na mataifa yaliyoendelea kuzishurutisha nchi changa kutekeleza sera zao ambazo si rafiki kwa utamaduni na uchumi wa nchi zinazoendelea (Khatibu, 1982; Chenoy, 1992). Hata hivyo, jamii za Kiafrika hazina budi kujenga uzalendo wa dhati

unaolenga kuuimarisha uchumi na utamaduni wa mataifa yao, kwa kuwa ndiyo msingi wa ustaarabu na maendeleo ya raia wake. Kwa hiyo, jamii haina budi kuacha tabia ya kuzipokea sera za kigeni bila kutathmini kwa kina ubora na udhaifu wake kwa ustawi na manufaa ya jamii za Kiafrika.

Mkangi katika riwaya ya *Walenisi* ameonesha jinsi nchi zinazoendelea, zikiwamo za Kiafrika, zilivyobadilika katika asili yake kutokana na kuiga mambo yaliyoletwa na Wakoloni. Aidha, Mkangi anaonesha jinsi jamii za Kiafrika zilivyoacha kuthamini utamaduni wao, ikiwamo lugha, dini, vyakula, mavazi, mila na desturi. Kulingana na namna hali inavyozidi kuendelea, jamii zinazidi kubadilika haraka, hasa kwa upande wa kudharau mila na desturi, lugha na tamaduni zao na kuthamini zile za kigeni (Sengo, 2009). Maadili ya jamii yanazidi kuporomoka kwa kasi hali inayosababisha asili ya Mwfrika kuzidi kufifia na kuangukia katika udhaifu wa kutojitambua, kama mwandishi anavyoeleza:

Ishara ya kifafa cha kutojijua kwa kawaida huleta matatizo na kuzua kisonono cha kuiga. Hali hii izukapo huwa mtu sio hajithamini yeze mwenyewe tu bali hata na ukoo wake wote, si jina lake, si utamaduni wake na si ustaarabu wake (Mkangi, 1995: 27).

Hali hii inajitokeza sana katika nchi za Kiafrika. Aidha, jamii za Kiafrika zimejisahau na hazithamini kabisa utamaduni wake wa asili. Utamaduni wa kigeni unautazama utamaduni wa Mwfrika katika udhaifu, kwa kuwa ule wa kigeni unapewa hadhi ya ubora na kipaumbele zaidi (Kavughya, 1997; Legulegu, 2016). Kwa mfano, Waafrika wanauia kujibadili ngozi na nywele ili wafanane na Wazungu. Hali hiyo ikiendelea, misingi na uendelevu wa utamaduni wa jadi katika nchi zinazoendelea utazidi kudhoofika na kusababisha kupotea kwa amali na tunu zilizomo kwa manufaa na uendelevu wa jamii na taifa kwa ujumla.

Kwa upande mwingine, Mkangi ameonesha jinsi ukoloni mamboleo unavyoathiri maendeleo ya jamii katika kila sekta na fani ya kimaendeleo katika nchi zinazoendelea zikiwamo za Afrika Mashariki. Mataifa yaliyoendelea yanazishurutisha nchi changa kutekeleza sera za kiuchumi ambazo hazina tija kwa nchi zinazoendelea (Chuachua, 2011). Sera hizo husababisha kuzorota kwa maendeleo ya umma, kwa kuwa zinalenga kunyonya rasilimali zilizopo kwa kutumia mbinu mbalimbali. Kwa mfano, mataifa yaliyoendelea hutoa masharti yasiyotekelzeza, yakiwamo ya kulima mazao ya biashara tu, jambo linalosababisha baa la njaa na wananchi kuangukia katika umaskini ambao haujawahi kufikiwa hata kabla ya ukoloni, kama Dzombo anavyoeleza:

Sikiliza we bwana Dzombo, usidhani hatujahusika. Mimi nimeshakueleza kwa nini mahindi yako ilibidi tuyafyeke. Na tulifanya hiyo, kwa sababu Benki ya Dunia yenye, ndiyo iliyotushauri kuwa sehemu hii inapaswa kupandwa mazao ya kutuletea pesa za kigeni (Mkangi, 1995: 18).

Katika dondo hili, mwandishi anaonesha namna mataifa ya kibepari yanavyozishurutisha nchi changa kimaendeleo kulima mazao ya biashara bila kuzingatia uwiano kati ya mazao ya biashara na chakula. Hapana shaka kuwa mazao ya biashara huuzwa kwa bei ya chini, ilhali pembejeo huuzwa kwa bei ya juu (Haji, 2003; Wamitila, 2003). Hali hii huwavunja moyo wakulima. Tahadhari isipochukuliwa, uchumi wa mataifa yanayoendelea utazidi kudhoofika na kuporomoka kabisa.

Athari za ukoloni mamboleo katika nchi zinazoendelea zikiwamo za Kiafrika zimeelezwa kwa undani katika riwaya hii ya *Walenisi*. Mkangi amemtumia Dzombo kudhihirisha jambo hili baada ya serikali kufyeka mahindi katika shamba lake. Serikali ilifyeka mahindi yote kwa kuwa ilikuwa imeagiza yapandwe mazao ya biashara tu. Wananchi katika jamii ya Dzombo hawakuruhusiwa kulima mazao ya chakula. Kwa bahati mbaya, mazao ya biashara yaliyopewa kipaumbele katika uzalishaji hayakuwa na tija kwa wananchi kwa kuwa yaliuzwa kwa bei ya chini ambayo haikuwiana na gharama za uzalishaji. Aidha, mazao ya biashara hayakupata soko la uhakika jambo lililosababisha wakulima kukopwa mazao yao na kutolipwa kwa wakati. Hali hii imesababisha wananchi wengi kuangukia katika umaskini na utegemezi katika nchi zilizoendelea kama Dzombo anavyoeleza:

Sasa nimwendee nani kueleza hali hii yangu? Sio kitambo mahindi yangu mliyafyeka na mkanishauri nilime haya yaletayo sijui pesa za kigeni...mlinigeuza na mimi na hata nikawa mwombaji wa hata hicho chakula chenyewe (Mkangi, 1995: 20).

Katika nkuu hii, mwandishi ameonesha athari za ukoloni mamboleo katika mataifa yanayoendelea hapa duniani. Kwa upande mwingine, mataifa ya kibepari hutumia mbinu mbalimbali ili kufanikisha lengo la kunyonya uchumi katika mataifa yanayoendelea. Baadhi ya mbinu hizo ni pamoja na kutoa misaada ya kijeshi, kiteknolojia, taasisi za kifedha, likiwamo shirika la Fedha la Dunia na Benki ya Dunia (Little, 1996). Mataifa hayo hulazimika kutoka nje ya mipaka yao ili kujiimarisha kimasoko na kimalighafi. Pia, hutumia mbinu za utengenezaji wa viongozi vibaraka ambao husimamia utekelezaji wa sera zao katika nchi zinazoendelea. Hali ya viongozi wa mataifa yanayoendelea kuwa vibaraka wa mataifa yaliyoendelea imechangia kwa kiasi kikubwa mataifa yao kujiingiza katika mikataba isiyo na tija kwa taifa (Ngadala, 2003).

Kulingana na Mvungi (1985) na Mayega (2006) usimamizi mbaya wa rasilimali za umma, uporaji na utoroshaji wa madini na uwiano wa mapato usioridhisha umeshuhudiwa katika miradi mingi iliyowekezwa hapa nchini na kwagineko barani Afrika. Pia, mwandishi ameonesha jinsi mataifa ya kipebari yanavyotumia mbinu za hali ya juu kuhakikisha masilahi yao yanatimizwa. Mataifa ya kibepari hujifanya kutenda wema kutoa misaada na hata kuchangia

shughuli za maendeleo huku yakitoa masharti magumu ya utekelezaji wa mikopo yatoayo (Njihia, 2005). Hali hii huyafanya mataifa ya kibepari kunyakua kila sekta ya kiuchumi katika nchi zinazoendelea zikiwamo za Afrika Mashariki na kwingineko barani Afrika. Wajibu wa viongozi katika nchi zinazoendelea ni kuziba mianya yote kwa kubuni mbinu mpya za kuzijengea uwezo nchi zao ili ziweze kujitegemea na kuepuka utegemezi.

Kwa ujumla, ukoloni mamboleo uliotamalaki katika nchi zinazoendelea ni tatizo linalohitaji viongozi kujikosoa na kuzisahihisha sera za uwekezaji ili kunusuru rasilimali za mataifa yao na kuwanasua wananchi mikononi mwa mabepari. Viongozi hawana budi kuzipokea sera za utandawazi kwa umakini kwa kufanya tathmini ya kina ya kiuchumi, kisera na kisheria kwa kuzingatia mahitaji sahihi ya taifa, kiwakati.

3.2 Matabaka katika Jamii

Matabaka ni dhana inayorejelea mgawanyiko katika jamii kutokana na kubaguana kwa misingi ya kidini, kipato, kikabila, kielimu, kijinsia, rangi na hata mahali atokapo mtu (Sengo, 1973). Matabaka ni chanzo cha matatizo mengi kwani baadhi ya watu hukosa huduma za msingi kutokana na kuwa na kipato cha chini (Hussein, 1988 na Shivji, 2006). Mkangi ameonesha athari za misuguano ya matabaka jinsi ilivyoshamiri katika nchi aliyokuwa anaishi Dzombo. Mwandishi analiangalia suala la matabaka namna linavyosababisha chuki, ukosefu wa haki, unyanyasaji, udhalimu na unyonyaji. Aidha, athari za matabaka zinajidhihirisha kwa namna mbalimbali katika jamii hasa ukichunguza uhusiano uliopo baina ya matajiri na maskini, kama mwandishi anavyodokeza:

Kwani kwa ghafla aliweza kuona vipande viwili nya miamba ya marasimu wa kwashakoo vimejikita njiani mwake. Miamba hii ilikuwa ya kitabaka. Hakutaka hata kusikia harufu za miamba hiyo. Aliuja kuwa ilikuwa ya kutoa harufu ya sumu kali kumfanya ainusaye kwa wingi kudhoofika akili milele. Sumu yenye ilitokana na ukosaji wa chakula bora. Kwa kawaida hali hii imezoeleka kwa wale walio ndani ya tabaka libebalo paa dogo, lakini sio zito. Utabaka ndiyo hueneza miamba hii (Mkangi, 1995: 23).

Mkangi katika dondo hili ameonesha jinsi tabaka la chini linavyokosa huduma za kimsingi, kama chakula na lishe bora kutokana na umaskini. Pia, anaonesha namna tabaka la juu linavyoweka mikakati ya kujiimarisha ambayo ina athari kubwa kwa wananchi wa tabaka la chini, kama mwandishi anavyodokeza kuhusu kuwapo kwa harufu ya sumu kali ya kumfanya ainusaye kwa wingi adhoofike milele. Matokeo yake, wananchi wanaangukia katika umaskini mkubwa. Hali hiyo husababisha idadi kubwa ya watoto wanaougua magonjwa ya utapiamlo hasa wale wanaoishi katika familia maskini (Ruhumbika, 1992). Hivi ndivyo, matabaka

yanavyosababisha kurudisha nyuma maendeleo ya jamii kutokana na kubaguana. Matabaka hayana budi kutokomezwa kwa kadiri jamii inavyoweza.

Pia, mwandishi ameleeza kuwa kukua na kukomaa kwa maendeleo ya viwanda katika nchi za Magharibi kumesababisha kuzuka kwa tabaka la mataifa yaliyoendelea na yanayoendelea. Mataifa yanayoendelea yamejenga utegemezi kwa mataifa yaliyoendelea. Hali hiyo ndiyo inayosababisha mataifa yanayoendelea yaendelee kufifia kiuchumi na kupewa masharti magumu yasiyoteklezeka. Utegemezi huo unapunguza thamani ya mataifa yanayoendelea kutokana na kuomba hata vitu vidogo ambavyo vingeweza kutengenezwa katika nchi zinazoendelea. Jambo hili linaleta aibu ya kudumu kwa nchi zinazoendelea zikiwamo za Kiafrika, kama mwandishi anavyoeleza:

Hapa ndipo kule kutokuwa na pesa kuzidipo kujidhihirisha kwa mwili mzima kupachikwa mabandeji ya msaada mwili mzima (Mkangi, 1995: 27).

Katika dondoo hili, mwandishi anakejeli suala la utegemezi uliokithiri ambao unatokana na mataifa yanayoendelea kutowajibika kikamilifu, pamoja na kuepu ka sumba ya kuendesha nchi kwa kutegemea uwezo wa wahisani. Hali hii inajibainisha pia kupitia bajeti za mipango ya maendeleo katika mataifa yanayoendelea ambazo zinategemea misaada kutoka kwa wahisani, yaani mataifa yaliyoendelea. Utegemezi huo unasababisha hata viongozi kutokuwa na nguvu ya kuji amini, kulinda rasilimali katika mataifa yao, kupewa masharti magumu katika mikataba ya shughuli za maendeleo, pamoja na kupangiwa bei za mazao na bidhaa nyinginezo. Kauli mbiu ya mwandishi ni kuvunja matabaka ya utegemezi kwa kujenga misingi ya uwezo wa kujitegemea katika ngazi ya familia, jamii na taifa.

Kadhalika, mwandishi ameonesha hali ya matabaka katika nchi ya Wachuna ambao wali amini kuwa watu hawawezi kuwa sawa hata siku moja, kwani wapo watakaokuwa na makazi bora, mavazi na wale watakaokosa kabisa. Pia, wapo wanaokosa hata mahitaji ya kawa idha na ya msingi katika jamii. Kwa mfano, baadhi hukosa matibabu, elimu, chakula ama mahitaji ya kila siku. Hata hivyo, wapo wanaomudu mahitaji hayo hata kuwa na uwezo wa kwenda kutibiwa au kusoma nje ya nchi. Nchi aliyoiishi Dzombo ilijengeka katika misingi ya matabaka ya matajiri na maskini na athari zake zilijibainisha waziwazi, kama mwandishi anavyoeleza:

Mafahari wawili hawakai zizi moja. Na wote wakielimika ni nani atatufulia chupi zetu? Kutusafishia magari yetu? (Mkangi, 1995: 173).

Katika nukuu hii, mwandishi ameonesha jinsi utegemezi unavyojenga matabaka katika jamii. Aidha, matabaka yanajenga makundi ya mabwana na watwana kama ilivyonukuliwa hapo juu. Mwachano mkubwa wa kitabaka unaoendelea baina ya mataifa yaliyoendelea na yanayoendelea, viongozi na wananchi, na kati ya matajiri na maskini ndio unaovunja utu wa binadamu na wengine kuwafanya waendelee

kunyanyaswa na kunyonywa katika mataifa mbalimbali ya dunia (Msokile, 1991; Mayega, 2006). Jambo la kuzingatia ni kwamba, mataifa yanayoendelea ama wananchi hawana budi kupata uvumbuzi wa kuchukua hatua za jinsi ya kuwajengea uwezo wananchi ili kupunguza pengo baina ya matajiri na maskini au kupunguza utegemezi mionganoni mwa mataifa yanayoendelea na yale yaliyoendelea zaidi katika nyanja za uchumi, sayansi na teknolojia.

Pia, mwandishi ameonesha namna watu wenye uwezo wanavyotumia nguvu zao za kiuchumi kuwanyonya na kuwakandamiza maskini. Dzombo na nduguye walifanya kazi kwa ujira mdogo usiulingana na kazi walizozifanya. Jambo hili limesawiriwa vyema katika nchi mbalimbali, hasa zinazoendelea, ambapo wakulima, wafanyakazi serikalini, viwandani na migodini wananyonywa kwa kupewa ujira mdogo usiulingana na unyeti wa majukumu yao, kwa mataifa yao (Nyerere, 1968). Hali hiyo, huzua migomo ya mara kwa mara kutohaka na mazingira magumu ya kazi, pamoja na mishahara midogo. Makala hii inatoa wito kwa serikali za nchi zote zinazoendelea kuyatokomeza matabaka katika utekelezaji wa maamuzi yanayonua kutetea masilahi ya wananchi kwa kupinga udhalimu ambao haupaswi kuvumiliwa.

3.3 Ukosefu wa Haki

Hadi nchi nyingi zinazoendelea barani Afrika zinapata uhuru mapema miaka ya 1960, ni wazi kwamba, zisingeweza kujenga misingi imara ya siasa na uchumi mara moja kwa kuwa sehemu kubwa ya rasilimali zake zilikuwa zimeporwa kwa miongo mingi na Wakoloni. Katika kipindi hicho, nchi nyingi zinazoendelea zikiwamo za Afrika Mashariki hazikufaulu kuondoa pengo la kuwapo kwa misuguano ya matabaka, ukiukwaji wa maadili ya uongozi na ukosefu wa usawa na haki lililojengeka tangu enzi za Ukoloni (Chuachua, 2011). Hata hivyo, mitazamo ya viongozi ililenga kuchukua hatua madhubuti za kuifanya nchi changa iweze kupiga hatua za kusonga mbele katika maendeleo yake, na wito kwa umma ukawa ni kuijenga jamii mpya itakayozingatia haki na usawa wa binadamu. Kwa hiyo, misingi ya uzalendo, uongozi imara, haki na usawa ilitegemewa katika kuzijenga na kuzilinda nchi zao.

Katika riwaya hii, Mkangi amezungumzia suala la haki jinsi linavyohusishwa na kufungamana na mhimili wa utawala na uongozi katika mataifa yanayoendelea. Mwandishi analichunguza suala la uongozi kama wakala wa haki katika jamii. Kwa mfano, uongozi mbaya hudhulumu haki za wananchi na kuwapuuza kama mwandishi alivyoonesha jinsi Dzombo alivyohukumiwa bila kupewa nafasi ya kujitetea. Viongozi wanaonekana kuwa wanyanyasaji, wadhulumaji na hutumia mabavu kuongoza wananchi wao. Viongozi hawatendi haki kwa wananchi wao. Dzombo baada ya kusema ukweli alifukuzwa kazi na baadaye kuhukumiwa kifo bila kupewa nafasi ya kujieleza au mashtaka

kusikilizwa kwa mujibu wa sheria kama zinavyouelekeza. Bila uhuru wa kujieleza taifa haliwezi kupiga hatua yoyote katika maendeleo yake, kwa sababu viongozi hawawezi kujikosoa na kujisahihisha kwa manufaa ya jamii na taifa.

Kwa upande mwingine, Mkangi ameonesha umuhimu wa kuwapo kwa uongozi unaozingatia misingi ya haki na demokrasia katika uendeshaji wa serikali. Mwandishi ameonesha namna suala la uongozi unaofuata misingi ya haki na uwazi ulivyojibainisha katika nchi ya Walenisi. Wawalenisi walikuwa wakifanya kazi kwa umoja na mshikamano baina ya viongozi na wananchi wao, kama anavyoueleza Mzee Utu Mwenzio:

Walenisi ilipata mwamko wa kimapinduzi uliokuwa chanzo cha mabadiliko makubwa, ndipo utu wa wananchi ulipochipuka. Utaratibu wa utawala wa Walenisi kwa ujumla, jukumu kubwa la viongozi lilikuwa kuyakabili matatizo yaliyopo na kuyatatua kwa lengo la kuimarisha utu (Mkangi, 1995: 147).

Kulingana na nukuu hii, Dzombo aliendelea kujifunza mifumo bora ya siasa za Walenisi, hatima yake aligundua kuwa utu ni kiini cha ufanisi na maendeleo yaliyotukuka katika nchi hiyo. Hali hiyo iliwafanya kufuta masuala ya dhuluma, matabaka, unyonyaji na uonevu katika nchi yao. Jambo hili ni adimu kupatikana katika nchi zinazoendelea hapa duniani. Mataifa haya yamekuwa na kawaida ya kuongoza kwa kutumia mabavu, kukiuka misingi ya kikatiba kwa kukatalia ukomo wa madaraka, dhuluma na kuwanyonya wananchi hasa wa tabaka la chini (Ngadala, 2003). Mwandishi ameitumia nchi ya Walenisi kama kijielezi kwa viongozi wa mataifa yanayoendelea ili yabadilike, wajisahihishe na kuiga mfumo wa kuongoza kwa kufuata haki, demokrasia na misingi iliyobainishwa katika katiba za mataifa yao.

Aidha, suala la ukosefu wa haki katika mahakama na mfumo mzima wa kutafsiri sheria katika vyombo husika linajadiliwa kwa kina katika riwaya hii. Haki ni uendeshaji wa jambo kwa kufuata sheria au kanuni zilizowekwa (TUKI, 2004). Mkangi anaonesha kuwa mahakama hazifuati haki na usawa kwani huzingatia sana upande mmoja wa mlalamikaji na kumnyima haki mshtakiwa. Kwa msingi huo, mahakama na vyombo vya dola kwa ujumla, hutazamwa kama nyenzo kuu inayofanya kazi kwa masilahi ya viongozi wa serikali zilizo madarakani. Vyombo hivyo vimepoteza uhalali na dhamira ya kuwa wakala wa umma kama inavyoiezwa kikatiba. Kwa mfano, Dzombo alihukumiwa kifo bila kupewa nafasi ya kujitetea, kama mwandishi anavyodokeza:

Dzombo hakutazamia huruma yoyote kutoka kwa hakimu...halikuwa jambo geni kuwa huruma za mahakimu hazitoki moyoni, bali kwenye kiini cha kudumisha maslahi yao (Mkangi, 1995: 1).

Hapa, mwandishi ameonesha namna wananchi wa kawaida, wakiwamo wakulima na wafanyakazi, wanavyonyimwa uhuru wa kujieleza, kutoa maoni na kutetea

masilahi yao. Kwa mfano, Dzombo alifukuzwa kazi baada ya kugundua ukweli kwamba ufukara wao ulitokana na kunyonywa na tajiri waliyekuwa wanamfanyia kazi. Udadisi wake wa kupenda kuhoji ndio uliomchonganisha na utawala wa jamii yake uliokuwa haupendi kukosolewa na kuweka mambo bayana. Dzombo alitazamwa kama mchochezi aliyehtarisha utulivu na usalama wa nchi. Wahanga wakubwa ni watu wa hali ya chini ambao hudhulumiwa haki ya kujitetea na kuhukumiwa bila makosa, kama mwandishi anavyoeyeza:

Yule hakimu aliegemeza miwani yake nusu glasi puaní kwake huku akimtazama kwa ile sehemu iliyokuwa wazi. Akamwamrisha kusimama. Zama hizo mahakama hazikuwa zikifuata sheria kwa mujibu wa kulinda au kudumisha haki za binadamu. Kazi yake kubwa ilikuwa ni kumtia hatiani aliyekuwa amepatwa na kisirani cha kushitakiwa kwa hatia bandia. Baada ya kusimama tu, hakimu naye bila kusita, akatamka, Kifo (Mkangi, 1995: 34).

Hivi ndivyo hakimu alivyomhukumu Dzombo ambaye hakupewa fursa ya kuzungumza lolote linalohusiana na kushtakiwa kwake wala kujitetea. Mwandishi anaonesha namna mahakama zinavyokiuka sheria na haki za binadamu kutokana na kiini cha masilahi yao binafsi. Hali hii inasababisha watu wengi kudhuluiwa haki zao za msingi. Ukosefu wa haki katika jamii unaathiri upatikanaji wa huduma sawa kwa jamii (Robert, 1967). Ukiukwaji wa haki za kiraia, kisanaa, kisiasa na kiutamaduni ndio unaosababisha maandamano, ghasia, vurugu, mauaji ya raia, pamoa na mapambano kati ya wananchi dhidi ya vyombo vya dola barani Afrika na kwingineko duniani (Mayega, 2006; Kabwe, 2016). Kwa hiyo, ustawi wa jamii na taifa lolote unategemea sana kuwapo kwa amani, utulivu, usawa na haki za binadamu.

Mwandishi amejadili suala la haki zinazohusu wanawake katika jamii. Ni jambo la kawaida kwa wanawake kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo na uzalishaji mali, lakini mchango wao katika maamuzi na mabadiliko ya uchumi na maisha ya jamii umeendelea kutambuliwa na kuthaminiwa kwa kiwango kidogo sana. Jambo hili limejengwa na mfumo wa utamaduni unaotawala ambao unamtazama mwanamke katika nafasi duni (Kajeza, 2016). Mtazamo huo huwafanya wanawake wabaguliwe katika shughuli za kijamii kutokana na kuwapo kwa mgawanyo usio sawa wa mamlaka katika nyanja za kijamii kama katika siasa, uchumi, jeshi na dini.

Mkangi amemchora mwanamke katika ncha mbili. Kwanza, kama mtu duni, na pili kama mtu mwenye hekima. Mwanamke anaonekana kama mtu asiye na haki ya kutoa maoni na kushiriki kikamilifu katika maamuzi yanayohusiana na maendeleo ya familia yake (Muhando, 1982). Kwa misingi hiyo, mwanamke amejengwa katika hali ya kupewa amri, kuamuliwa na kutii au kupokea amri kutoka kwa mumewe. Mara zote mwanamke ameonekana kuwa ni mtu wa kutukanwa na kuonewa, kama mwandishi anavyoeyeza:

Ikiwa aliambiwa azae, basi atazaa kama mtambo. Alipomwambia asizae, basi hapo mataabisho ya tembe, sindano na vijiti vilipogunduliwa wengi walifanywa tasa na mifereji ya mayai ya uzazi kukatwa (Mkangi, 1995: 123).

Katika nukuu hii, mwanamke amejengwa kama mtu wa kusikiliza na kutenda tu yale anayoamriwa na mumewe. Haruhusiwi kusema chochote, kudadisi au kuhoji. Jambo la msingi katika nukuu hii ni kwamba, wanawake waheshimiwe, wasikilizwe na mawazo yao yathaminiwe. Aidha, ni wakati sahihi wa kuunda sheria zinazotekelzeza na zinazolenga kupambana na kuondoa mianya inayomdhulumu mwanamke katika sekta zote za kijamii, vinginevyo, nafasi yake itaendelea kuwa duni katika maamuzi na majukumu ya kijamii na kitaifa (Moi, 1985).

Hata hivyo, udhaifu unaoelezwa kuhusu wanawake unatazamwa tofauti na Abdun (2000) anayeeleza kwamba, mwanamke ni nguzo katika kukuza uchumi wa familia, jamii na taifa. Anaendelea kueleza kwamba, hakuna asiyefahamu kuwa mwanamke ni nguzo kuu ya uzalishaji mali na uchumi hapa nchini. Jamii itambue kwamba, kumuelimisha mwanamke ni njia mojawapo ya kuiokoa jamii katika dimbwi la umaskini; ingawa, kimsingi, elimu ni haki ya lazima kwa kila mtu bila kujali jinsia. Kwa upande mwingine, Mkangi amemchora mwanamke kama kitovu cha hekima, kama anavyooleza Mama Mtu Maanani kuwa:

Sasa mwanamke amekuwa kitovu cha hekima na kuwa suala hili wanawake wote wanalifurahia (Mkangi, 1995: 23).

Hapa, upekee wa nafasi ya mwanamke katika jamii umeelezwa waziwazi. Ni jambo la kawaida kwa wanawake kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo na uzalishaji mali, lakini mchango wao katika maamuzi na mabadiliko ya uchumi na maisha ya jamii umeendelea kutambuliwa na kuthaminiwa kwa kiwango kidogo sana (Matundura, 2008). Jambo hili limejengwa na mfumo wa utamaduni unaotawala ambao kwa muda mrefu umeendelea kudhulumu haki ya msingi ya mwanamke (Bond, 2000 na Mamonyi, 2001). Mtazamo huu ni mojawapo ya matokeo ya tabia na desturi zenye ubaguzi wa kijinsia zilizotamalaki katika jamii ambazo hazina budi kupingwa kijamii, kitaifa na kisheria.

Kwa ujumla, katika kupigania haki za msingi za kiraia hapa nchini, elimu kuhusu haki za wanawake na binadamu kwa ujumla, utamaduni na uchumi havina budi kupewa kipaumbele ili wananchi wawajibike kulingana na mahitaji yao kiwakati. Dzombo aliishi katika nchi yenye udhalimu na umaskini uliokithiri na raia wake hawakujua chanzo chake, kwa sababu hawakuwa na elimu ya kutambua haki zao na namna sahihi ya kukabiliana na matatizo yaliyokuwa yakiwasibu. Hata hivyo, Dzombo alipata mwamko na uvumbuzi wa matatizo yaliyokuwa yanaisibu nchi yake, na aliamua kwenda kuikomboa.

4.0 Hitimisho

Mkangi kupitia riwaya ya *Walenisi*, kwa kiasi kikubwa, amefaulu kueleza hali halisi iliyoakisiwa katika nchi nyingi zinazoendelea, zikiwamo za Afrika Mashariki na kwingineko barani Afrika. Baadhi ya mambo hayo yanahu su misuguano ya kitabaka, ukosefu wa haki, pamoja na athari za ukoloni mamboleo kama yalivyoelezwa katika makala hii. Wito wa makala hii ni kwamba, viongozi wawe wepesi kujenga misingi imara inayoteklezeka inayolenga kujikosoa, kujisahihisha, pamoja na kuchukua hatua za kupambana na matatizo yanayoziandama nchi zao. Kwa hakika matatizo hayo, kwa kawaida, yanaathiri kila fani ya maendeleo katika nchi mbalimbali. Kwa hiyo, wajibu wa viongozi ni kujenga misingi imara itakayowawezesha wananchi na mataifa kujitegemea kiuchumi, pamoja na kulinda tunu na amali za mataifa kwa manufaa ya mataifa na raia wake.

Marejeleo

- Abdun, N.H. (2000). *Ukombozi wa Mwanamke*. Morogoro: Mzumbe Book Project.
- Bond, S. (2000). Culture and Feminine Leadership, *Women Power and the Academic from Rhetoric to Reality*. New York: Berghahn Books, pp. 67-83.
- Chenoy, A.M. (1992). *Urusi Mwezi Kufikiri Juu ya Harakati za Ukombozi wa Kiafrika: Mwendelezo*. London: Cambridge University Press.
- Chuachua, R. (2011). *Itikadi katika Riwaya za Shaaban Robert*. Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.
- Haji, G.H. (2003). *Kimbunga*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.
- Hussein, E.N. (1988). *Kwenye Ukingo wa Thim*. Nairobi: Oxford University Press.
- Idrissa, J. (2016, Desemba 3-9). Waliozoea Dhuluma Waache Yaishe, *MwanaHalisi*. Na. 176, uk. 15.
- Ipara, I.O. (2003). *Mwongozo wa Walenisi*. Eldoret: Western Educational Publishers.
- Kabwe, Z. (2016, Agosti 15-21). Dalili za Udikteta Zinaposhamiri, *MwanaHalisi*. Na. 352, uk. 4.
- Kajeza, T. (2016). Usawiri wa Mwanamke katika Fasihi Andishi: Mifano katika Riwaya ya *Machozi na Damu* (2005) ya E. Shigongo. Tasinifu ya Shahada ya Kwanza. Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira, Mbeya (Haijachapishwa).
- Kavugha, F.S. (1997). *Desturi na Mila za Wapare*. Soni: Vuga Press.
- Khatibu, S.M. (1982). *Pambazuko la Afrika*. Arusha: East Africa Publication Ltd.
- Legulegu, S. (2016). Siasa na Uchumi katika Fasihi ya Kiswahili. Tasinifu ya Shahada ya Kwanza. Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira, Mbeya (Haijachapishwa).
- Little, A. (1996). Globalization and Education Research: Whose Context Counts?, *International Journal of Development*, 16 (4): 427-438.

- Makoye, H. (1996). Tanzania Traditional Dances, Choreography and Communication in Urban. A Research Report of the Requirement for the Master Degree (Unpublished). Dar es Salaam: University of Dar es Salaam.
- Matundura, B. (2008). *Sitaki Iwe Siri*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- Mayega, P. (2006). *Mwalimu Mkuu wa Watu*. Dar es Salaam: MBP Enterprises.
- Mgogo, Y. (2012). Matumizi ya Nyimbo za Wanyiha Misibani. Tasinifu ya Shahada ya Uzamili. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. (Haijachapishwa).
- Mihanjo, A. (2010). *Falsafa na Ufunuo wa Maarifa*. Morogoro: Turiani.
- Mkangi, K. (1995). *Walenisi*. Nairobi: Focus Publications Limited.
- Moi, T. (1985). *Sexual/Textual Politics: Feminist Literary Theory*. London: Routledge.
- Momanyi, C. (2001). Nafasi ya Mwanamke katika Ushairi wa Shaaban Robert, *Kiswahili*, kur. 53 - 65.
- Msokile, M. (1991). *Uchambuzi na Uhakiki: Lina Ubani*. Dar es Slaam: Dar es Salaam Publishers Press.
- Muhando, P. (1982). *Nguzo Mama*. Nairobi: Oxford University Press.
- Mvungi, T. (1985). *Chungu Tamu*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.
- Ngadala, D.K. (2003). Ujenzi na Mmomonyoko wa Maadili ya Taifa: Mkutano wa Sekta ya Utamaduni. Morogoro.
- Njihia, S.K. (2005). Kiswahili na Utandawazi, *Insha za Jubilei, Utandawazi na Umoja wa Afrika*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. kur. 51 – 58.
- Nyerere, J.K. (1974). *Binadamu na Maendeleo*. Dar es Salaam: Oxford University Press.
- _____. (1968). *Ujamaa*. Dar es Salaam: Oxford University Press.
- Robert, S. (1967). *Kusadikika*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.
- Ruhumbika, G. (1992). *Miradi Bubu ya Wazalendo*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.
- Sengo, T.S.Y. (2009). *Sengo na Fasihi za Kiinchi*. Dar es Salaam: The Registered Trustee of Al-Amin Education and Research Academy.
- _____. (1993). *Fasihi Simulizi ya Mtanzania*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Shivji, I. (2009). *Accumulation in an African Periphery*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.
- TUKI (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.
- Wamitila, K.W. (2003). *Bina – Adamu*. Nairobi: Focus Publications Limited.
- _____. (1995). *Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Focus Publications Limited.